

“Sikiliza” Lugha ya Ishara!

Je, unajua kuimba?

Unaweza kuimba “Mwabudu Yehova Ujanani,” wimbo namba 41, kutoka katika kitabu *Mwimbieni Yehova?* Tafuta wimbo huo katika kitabu chako cha wimbo, au pakua maneno ya wimbo huo kutoka jw.org/sw. (Angalia chini ya MACHAPISHO > VITABU NA BROSHUA.) Maneno ya wimbo huo yanakukumbusha kuwaheshimu wazazi wako na kumsikiliza Yehova Mungu.



Je, unajua jinsi viziwi wanavyoimba?

Wanatumia lugha ya ishara. Tazama wimbo “Mwabudu Yehova Ujanani” katika Lugha ya Ishara ya Marekani kwenye jw.org/sw. (Angalia chini ya MACHAPISHO > LUGHA YA ISHARA. Hakikisha unachagua Lugha ya Ishara ya Marekani.) Ona ikiwa unaweza kukisia maana ya baadhi ya ishara hizo.

- **SASA JARIBU KUFANYA HIVI:** Omba mtu mmoja katika familia achague andiko analolipenda sana kutoka kwenye Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo (Mathayo mpaka Ufunuo). Someni pamoja andiko hilo na kisha mtu mmoja katika familia ajaribu “kusoma” andiko hilo kwa kutumia ishara tu. Kisha, tazameni jinsi andiko hilo linavyosomwa katika Lugha ya Ishara ya Marekani kwenye jw.org/sw. (Angalia chini ya MACHAPISHO > LUGHA YA ISHARA. Hakikisha unachagua Lugha ya Ishara ya Marekani.) Je, mnaweza kufuatana na usomaji huo?